FIKIRIA

KANUNI ZA UADILIFU ZA SGS

WENZANGU WAPENDWA,

Uadilifu uko katika kitovu cha Kundi la SGS. Imani tunayowapa wateja na washika dau wetu ndio ufunguo wa mafanikio yetu kama shirika na pia kama watu binafsi.

Kama viongizi katika sekta yetu, tunajiweka katika kiwango cha juu sana cha maadili ya kitaaluma. Kanuni zetu za Uadilifu ni dhihirisho la maadili yanayoshirikishwa kote SGS, biashara zake na washirika wake mbalimbali.

Ili kutimiza malengo yetu, tunalenga kuvutia na kuwashikilia wafanyikazi walio na moyo wa kufanya kazi zao kwa uongozi, kwa haki na uaminifu. Tunatambua ya kwamba tuko na wajibu kwa kila mmoja wetu na kwa wateja wetu kutekeleza kanuni zetu za uadilifu.

Sisi ndio watunzaji wa chapa na heshima ya SGS na tunaendelea kujitahidi kulinda thamani zinazowakilisha kwenye sehemu za masoko. Tutafikia lengo hili kwa kufanya biashara yetu kwa uaminifu na uwazi. Kama sehemu ya ahadi hii, tunahimiza utamaduni wa uwazi tunaoweza kibadilishana dhana na taarifa, kutafuta mawazo na kueleza matatizo, bila woga wa ulipizi.

Hii inaturuhusu kuhudumia matakwa ya wateja wetu sokoni tunapochagua kufanya kazi, kutoa fursa kwa wafanyikazi wetu na kutengeneza faida endelevu kwa wenye hisa.



Peter Kalantzis
Mwenyekiti wa Bodi

Frankie Ng
Afisa Mtendaji Mkuu

SGS ndiyo kampuni inayoongoza duniani katika ukaguzi, uthibitisho, upimaji na utowaji wa vyeti. Ilianzishwa mwaka wa 1878, kwa sababu ya hitaji la wanunuzi na wauzaji kutegemea mshiriki wa tatu aliye huru, wa kweli na mwaminifu asimamie usafirishaji wa nafaka. Leo, ingawa SGS imekuwa na imeingia sekta zingine za utaalamu, bado inaendelea kutimiza wajibu wa mshiriki wa tatu mtaalamu na aliye huru anayeweza kutegemewa na wachuuzi, wazalishaji, wanunuzi na pia serikali.

Mafanikio ya SGS yanategemea imani inayopata kila siku kutoka kwa wanunuzi, wafanyikazi, wenye hisa na kutoka kwa jumuiya inapofanyia biashara.

Imani hii imepatwa kupitia bidii za pamoja za vizazi vya wafanyikazi wa SGS. SGS inalenga kudumisha imani hii kwa utekelezaji unaofaa wa Kanuni hizi za Uadilifu.

UTUMIAJI WA KANUNI

Kanuni hizi zunawahusu wafanyikazi wote, maafisa na wakurugenzi wa SGS na makampuni shiriki. Vipengele vyote vya Kanuni, ambavyo havihusiani na wafanyikazi wa SGS, lazima pia vizingatiwe na makandarasi, washauri, wafanyikazi huria, wambia wa miradi ya pamoja, washenga, makandarasi wasaidizi na mtu yoyote anayetenda kwa niaba ya, au anayewakilisha, SGS.

KUELEWA KANUNI

SGS imejitolea kwa desturi ambayo mambo ya uadilifu na kanuni za kitaalam zinaweza zikadakizwa na kujadiliwa kwa uwazi. Ushauri na usaidizi unapatikana kusaidia wafanyakazi kuelewa Kanuni na kuwasaidia wafanye uamuzi uliosawa wanapokumbana na mtanziko wa maadili.

HAKUNA ULIPIZI KWA RIPOTI ZA NIA NJEMA

Wafanyikazi wanahimizwa waongee na waripoti mashauku yoyote au tuhuma zozote kwamba Kanuni zinavunjwa. SGS inahakikisha kwamba hakuna mtu yoyote anapitia aina yoyote ya malipizi au matokeo ya adhabu kwa sababu ya kutafuta ushauri au kuripoti ukiukaji wa Kanuni. Ulipizi kwa mfanyikazi ambaye ameripoti ukiukaji kwa nia njema yatasababisha adhabu.

UTAMADUNI WA UADILIFU

MAADILI YA UADILIFU YA SGS

- **IMANI:** hii ndio rasilimali yetu moja inayothaminiwa sana, msingi wa chapa na sifa yetu. Wateja wanategemea uadilifu wetu na imani hii inafaa kukuzwa na kulindwa siku baada ya siku. Inaweza hatarishwa haraka.
- **UAMINIFU NA UWAZI:** kwa kila kitu tufanyacho, tufaa kuwa watu wa kweli kwetu wenyewe, kwa wateja wetu na wafanyikazi wenzetu. Hakuna hali inayo halalisha uwongo, ulaghai au ukosefu wa uaminifu.
- **UWAJIBIKAJI:** kila ya matendo yetu na kutotenda kwetu kuna matokeo. Tunakubali matokeo ya chaguzi zetu na hatulaumu wengine kwa matendo yetu.
- **MAADILI:** tunaamini utendaji wa uadilifu, usawa na heshima kwa watu wengine. Maamuzi yetu yataongozwa na heshima kwa maadili na viwango vya tabia nzuri, na sio kwa maamuzi ya kiholela au upendeleo wa kibinafsi.

JIULIZE MASWALI ADILIFU

- Je, ninashuku kwamba kitendo Fulani kinaweza kuwa cha haramu au kisichokuwa cha maadili?
- Itaonekana aje kama uamuzi huu utaripotiwa kwa gazeti, au kama nitaongea kuhusu jambo hili na familia yangu na marafiki?
- Je, kitendo kinachopendekezwa kinahusu udanganyifu au kutokuwa na ukweli?
- Je, kitendo kinachopendekezwa kinaweza kuhatarisha usalama au afya ya mtu binafsi au watu wengine?
- Kitendo kinachopendekezwa kinaweza kuharibu SGS au sifa yake?
- Kitendo hicho kiko na madhumuni ya biashara yaliyohalali?

Kama kitendo kinachopendekezwa hakitafaulu jaribio lolote la majaribio haya, lazima utafute ushauri na ufikirie tena uamuzi wako.

UKIUKAJI HAUTAVUMILIWA

Uvunjaji wowote wa Kanuni, uwe mdogo aje, unaweza ukadhuru sifa na chapa ya SGS na hautavumiliwa. Ukiukaji Kanuni utasababisha kitendo cha adhabu, ikiwa ni pamoja na kuwachishwa kazi na mashtaka ya jinai kwa ukiukaji mkubwa.

KUTAFUTA USHAURI AU KUDAKIZA MATATIZO

Wakati wa tashwishi kuhusu maana ya Kanuni au matumizi yake katika hali bayana, wafanyikazi wanafaa wajadili jambo hili na msimamizi au meneja wao, idara ya Rasilimali Watu au na idara ya kisheria ya SGS. Maelezo ya mawasiliano ya rasilimali za kisheria za SGS yanaweza patikana katika wavitu wa ndani. Wafanyikkazi wanaweza pia wakajadili jambo lolote linalohusiana na Kanuni hizi na wakaguzi wa ndani.

Kama haiwezekani au haifai kwa mfanyikazi kueleza tatizo kwa usimamizi wa kazi yake, anaweza kuwasiliana na Afisa Mkuu wa Uzingatiaji wa SGS. Wafanyikazi wanaowezajua kuhusu ukiukaji au wanashuku ukiukaji wa Kanuni wanahimizwa kuripoti kwa Afisa Mkuu wa Uzingatiaji wa SGS.

Wafanyikazi wa SGS wa sasa na wa awali, na wateja au wagawaji, au mtu wa tatu wanaweza kuwasiliana na Afisa Mkuu wa Uzingatiaji wa SGS kuhusu mambo yanayohusiana na Kanuni za Uadilifu kupitia njia yoyote kati ya njia zifuatazo:

- Posta: SGS SA / kwa Afisa Uzingatiaji Mkuu wa SGS/ 1 place des Alpes, Sanduku la Posta 2152, CH – 1211 Geneva 1
- integrityhelpline.sgs.com
- Simu au Faksi:

  t +41 (0)22 739 91 00

  f +41 (0)22 739 98 81 (simu zinajibiwa wakati wa masaa ya kazi ya Geneva)
- Laini ya Usaidizi wa Uadilifu ya SGS: +1 800 461-9330 (namba/laini ya simu isiyolipishwa ada iliyowazi masaa 24, kila siku)

Laini ya Usaidizi wa Uadilifu ya SGS inaendeshwa na mtoa huduma aliye huru aliyebobea katika ushughulikiaji wa matatizo yanayohusiana na uzingatiaji na maadili. Kwa mara nyingi, mtu anayepiga simu kwa Laini ya Usaidizi wa Uadilifu ya SGS anaweza kuongea na mpokeaji simu na apokee majibu kwa lugha yake. Mawasiliano yanayofanywa kwa Laini ya Usaidizi wa Uadilifu ya SGS yanawekwa kwa usiri na yanaripotiwa kwa Afisa Mkuu wa Uzingatiaji wa SGS anayelinda, wakati kunahitajika, kutojulikana kwa mtoa habari.

Wakati Afisa Mkuu wa Uzingatiaji wa SGS, meneja wa Rasilimali Watu, mkaguzi wa ndani au wakili wa ndani wa SGS anafikiwa na mawsiliano kuhusu Kanuni za Uadilifu, habari inayotolewa inawekwa kama ya siri na inatumiwa kujibu au kushughulikia jambo lililoelezwa peke yake. Watu wanaotoa ripoti wanahimizwa wapeane majina yao na maelezo ya mawasiliano lakini wanaweza kuamua kutopeana majina. Kwa hali hii, njia inayofaa ya kuwasiliana inawezabuniwa kumruhusu mpiga simu apokee majibu bila kuhusisha utambilisho wake.

Tuhuma za uvunjaji wa Kanuni za Uadilifu zinazofikishwa kwa Afisa Mkuu wa Uzingatiaji wa SGS zinachunguzwa kwa usawa. Inapofaa, jibu la matokeo ya uchunguzaji linawasilishwa kwa mtu anayelalamika au anayeripoti.

UADILIFU WA HUDUMA

Huduma zote za SGS lazima zifanywe kwa utaalamu na kwa uaminifu kulingana na viwango, utaratibu na sera zilizokubaliwa. SGS inadumisha uhuru wake wa maoni na haikubali msukumo wa ushurutisho na vishawishi ili kutafsiri matokeo vibaya au kubadilisha matokeo ya uchunguzaji wake, utoaji vyeti, ukaguzi au majaribio yake. Matokeo yote lazima yanakiliwe kikamilifu na hakuna ripoti au vyeti visivyo vya kweli au vya kupotosha vitatolewa.

Matokeo yote lazima yanakiliwe sawasawa na yasibadilishwe kwa njia isiyofaa. Matokeo na maoni yanayotolewa na SGS yanaungwa mkono na faili za kazi na ripoti za shughuli zilizo za kweli na sahihi zinazowekwa kulingana na sera husika za Kundi la SGS.

UKAMIILIFU WA REKODI ZA KIFEDHA

Taarifa inayoandikwa katika rekodi za kifedha za SGS lazima iwe ya ukweli na haki, ya wakati wa kufaa na sahihi. Shughuli zote lazima zirekodiwe vizuri na sawasawa na maingizo kwa vitabu vya hesabu lazima yalingane na nyaraka sahihi zilizotolewa na washiriki halali.

Rekodi zote lazima ziwekwe kulingana na sheria na sare husika za Kundi la SGS.

MIVUTANI YA MASLAHI

MIVUTANO YA MASLAHI: KWA UJUMLA

Mivutano ya maslahi, au kuonekana kwa uwezekano wa mivutano ya maslahi, lazima iepukwe. Wafanyikazi wa SGS wanatarajiwa kuarifu meneja wao (au kuarifu Afisa Mkuu wa Uzingatiaji) mara tu wanapojua kwamba maslahi yao ya kibinafsi au maslahi ya kibinafsi ya jamaa wao wa karibu au marafiki wa karibu yanauwezo wa kutofautiana na maslahi ya SGS.

Mvutano wa maslahi unatokea wakati fursa ya mfanyikazi ya kujinufaisha inaweza ikazuia uamuzi wake, usawa, uhuru au utiifu wake kwa SGS.

Hayo yanajitokeza pale jamaa wa karibu au marafiki wa karibu wa mfanyikazi wa SGS wako na shughuli au maslahi yanayotofautiana na SGS.

Mivutano ya maslahi inaweza ikaanza kwa njia nyingi tofauti. Kama kuna tashwishi, wafanyikazi wanafaa kutafuta ushauri.

Wafanyikazi lazima waseme mara moja kwa maandishi mivutano yote ya maslahi inayoweza ikatokea kwa meneja wao na waache kujihusisha na mchakato wa uamuzi almradi wanaathiriwa na mvutano wa maslahi unaowezekana.

JAMAA WA KARIBU: UFAFANUZI

Jamaa wa karibu wa mfanyikazi ni pamoja na: mume/mke au mwenzi wa maisha; watoto, wajukuu; wazazi; babu/bibi; ndugu; shemeji/wifi; wakwe; na mtu yoyote anayeishi na mfanyikazi. Wakati unaofaa, washirika wa SGS wanaweza kutoa sera ya mahali inayorefusha orodha hii kwa jamaa wengine ili wazingatie mila za mahali.

IDHINI YA AWALI INAHITAJIKA

Mivutano ingine ya maslahi inayowezekana inayowakumba wafanyikazi wa SGS inaweza kutatuliwa na idhini ya awali na ruhusa inayofaa ya SGS. Hii ni pamoja na:

Ukurugenzi nje ya SGS

Kuhudumu katika bodi ya wakurugenzi ya kampuni nje ya SGS, kuhudumu katika bodi ya ushirika wa wataalamu au biashara au kutwaa uteuzi wa kisiasa wa mahali pa karibu au wa kitaifa kunahitaji idhini ya awali ya Afisa Mkuu wa Uzingatiaji wa SGS (kwa wajembe wa Halmashauri ya Uendeshaji kunahitaji idhini ya awali ya Kamati ya Maadili ya Kitaaluma).

Kufanya kazi nje ya SGS

Kuchukua kazi ya pili au ajira nje ya SGS kunahitaji idhini ya awali iliyoandikwa kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa mshirika na Meneja wa Rasilimali Watu wa Eneo. Lakini, hali zifuatazo haziruhusiwi: (i) kumfanyia mteja wa SGS kazi ambapo mfanyikazi anafanya kazi wakati wa ajira yake kwa SGS; (ii) kumfanyia mshindani wa SGS kazi; au (iii) kufanyia kampuni inayosambazia SGS bidhaa na huduma.

Kuajiri jamaa ya karibu

Kuajiri jamaa wa karibu wa mfanyikazi wa SGS aliopo kunahitaji idhini cha awali iliyoandikwa kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa mshirika na Meneja wa Rasilimali Watu wa Eneo. Ikizidi, kuajiri jamaa wa karibu wa wajembe wa Halmashauri ya Uendeshaji, au wakurugenzi wakuu wa mshirika wa SGS na wa ripoti zao za moja kwa moja, kunahitaji idhini ya awali iliyoandikwa kutoka kwa Afisa Mkuu wa Uzingatiaji.

Hakuna hali yoyote ile ambapo mfanyikazi wa SGS ameruhusiwa kuajiri, kusimamia au kushawishi makubaliano na masharti ya ajira ya jamaa wa karibu.

YASIORUHUSIWA

Hali zingine za mivutano ya maslahi zimepigwa marufuku kwa wafanyikazi wa SGS. Hizi no pamoja na:

Kijunufaisha

- Kutoa au kushiriki mwenyewe katika aina yoyote ya huduma za kitaalamu au ushauri kwa mteja au mteja anayetazamiwa wa SGS.
- Kushindana na SGS au kumfanyia mshindani wa SGS kazi.
- Kujipatia manufaa ya kibinafsi, au kumpatia jamaa wa karibu manufaa ya kibinafsi, kwa kutumia vibaya cheo ndani ya SGS au kufikia habari za SGS.

Uwekezaji wa kibinafsi na wagawaji, washindani na wateja

- Kutumia, huku akijua, huduma za mgawaji au mkandarasi msaidizi wa SGS ambapo mfanyikazi au jamaa wa karibu, moja kwa moja au kupitia mtu mwingine, ako na kiasi muhimu cha hisa au manufaa mengine ya kifedha hakuruhusiwi, ila: (i) mvutano unaowezekana umeelezwa kwa uwazi kwa meneja wa laini ya mfanyikazi na (ii) mfanyikazi aliyeathiriwa na mvutano hashughuluki na mchakato wa ununuzi.
- Uwekezaji wa kibinafsi na mgawaji, mkandarasi msaidizi, mshindani au mteja wa SGS hauruhusiwi, ila kwa njia ya kununua hisa katika soko la hisa la umma.

UTUMIAJI WA MALI NA RASILIMALI ZA KAMPUNI

LINDA MALI YA KAMPUNI NA FEDHA

Wafanyikazi wa SGS wako na wajibu wa kulinda na kutumia mali na fedha za kampuni zilizo chini ya usimamizi wao kwa njia inayofaa. Utumiaji wa mali au rasilimali za SGS kwa manufaa yoyote ya kibinafsi au kufanya kazi kwa mtu wa nje hakuruhusiwi.

UTUMIAJI WA RASILIMALI ZA TEKNOLOJIA YA MAWASILIANO

Kompyuta, mfumo wa mtandao na vyomo vya kuwasiliana vya kielektroni vya kampuni lazima vitumiwe kwa madhumuni ya kitaalamu, kwa kulingana na sera za SGS. Kutumia barua pepe, mtandao na aina nyingine za mawasiliano ya kielektroni kunaweza kukafuatiliwa na kukaguliwa na SGS (panaporuhusiwa na sheria husika za faragha) wakati tuhuma za matumizi mabaya inazuka.

UNUNUZI

Wafanyikazi wa SGS wanaohusika na ununuzi wa bidhaa na huduma kutoka kwa wagawaji au uchaguaji wa makandarasi wasaidizi lazima wafanye hivyo wakiwa na lengo moja la kuhakikisha thamani nzuri kwa hudumu hizo, wakizingatia ubora na sifa za mgawaji. Kwa wakati unaofaa, lazima bei zenye ushindani zichaguliwe kabla ya kuchagua mgawaji au mkandarasi msaidizi. SGS haipeani mikataba kwa wagawaji kwa msingi wa upendeleo wa kibinafsi. Uombaji wa aina yoyote ile ya mafao ya kibinafsi kutoka kwa mgawaji au kutoka kwa mtu anayetaka kutoa huduma kwa SGS umepigwa marufuku kabisa.

UTOAJI HONGO NA UFISADI

UTOAJI HONGO NA UFISADI

SGS haijishirikishi na utoaji hongo au ufisadi wa aina yoyote, katika nchi yoyote ambako inaendesha biashara. Wafanyikazi, au mtu yoyote anayetenda kwa niaba ya SGS, hapaswi kutoa au kulipa pesa kwa maafisa wa serikali, ikiwa ni moja kwa moja au kupitiakwa mtu mwingine, au kuwapatia aina yoyote ya zawadi au burudani wakiwa na lengo la kushawishi uamuzi wao, au kuwahamasisha kuipatia SGS manufaa yasiyofaa. Hii pia inatumika kwa maafisa na wafanyikazi wa mashirika ya kibinafsi.

Mfanyikazi yoyote wa SGS anayepokea madai ya hongo lazima aripoti jambo hilo mara moja kwa meneja wa laini yake na/au kwa Afisa Mkuu wa Uzingatiaji wa SGS.

HAKUNA MALIPO ILI KUPATA BIASHARA

SGS hailipi au haipeani aina yoyote ya motisha usiofaa kwa madhumuni ya kuipatia SGS bishara.

WASHENGA NA WASHAURI

SGS haishirikishi huduma za watu wa tatu kutoa hongo, asilimia ya faida haramu au bahashishi kwa niaba yake.

SGS haitumii huduma za washenga, wakala, washauri, wambia, wambia wa biashra ya pamoja au makandarasi katika kesi ambazo inashuku kwamba wambia hao wanaweza shiriki karika ufisadi au matendo mengine ya biashara haramu. Hakuna mshega au wakala wa uuzaji anaweza kushirikishwa ila tu mchakato wa juhudi unaofaa umefanywa kukadiri kufaa kwao na kama malipo ya mshenga yanalingana na huduma anazotoa. Ombi la kuajiri mshenga lazima liungwe mkono na mjumbe wa Halmashauri ya Uendeshaji la SGS na liidhinishwe na Kamati ya Maadili ya Kitaaluma. Washenga lazima wapatiwe, wapige sahihi na wakiri nakala ya Kanuni hii na wakubali kufanya kazi kwa maadili yake katika hali zote sa uhusiano wao na SGS. Wafanyikazi wa SGS wanaosimamia utumizi wa mshenga wako na wajibu wa kufuatilia mara kwa mara uzingatiaji wao wa Kanuni.

MALIPO WA URAHISISHAJI

Malipo ya urahisishaji ni malipo yanayolipwa mara moja tu ya thamani ya wastani yanayotolewa kwa ajili ya kuharakisha au kurahisisha utendaji wa afisa wa umma wa cheo cha chini kwa kitendo cha kawaida ambacho kisheria ni haki ya SGS. Madai kutoka kwa maafisa ya malipo ya urahisishaji lazima yakataliwe kabisa na yakubaliwe tu wakati kukataa kunaweza leta madhara kwa hali ya wafanyikazi au kunaweza kuleta hatari kubwa kwa biashara ya SGS.

KURIPOTI NA UHASIBU

Katika hali za mara chache pale malipo ya urahisishaji yanapswa kulipwa, mfanyikazi anayefanya au anayeidhinisha malipo lazima atoe ripoti kwa kuandika kwa nini malipo hayangeepukwa, kiasi kilicholipwa, tarehe na risiti ya malipo. Malipo ya urahisishaji lazima yahesabiwe kwa njia ambayo inaruhusu yakaguliwe. Ikitegemea utendaji na sheria za mahali, washirika wa SGS wanaweza tekeleza sheria za undani na zenye vikwazi vingi au wazuie wafanyikazi kutolipa malipo hayo ya urahisishaji.

HAKUNA MATOKEO MABAYA YA KUKATAA KULIPA HONGO

Hakuna mfanyikazi wa SGS ataadhibiwa kwa kukataa kulipa hongo, kwa kukataa kushiriki katika matendo ya ufisadi au kukataa kulipa malipo ya urahisishaji.

MICHANGO YA KISIASA NA MICHANGO YA KIMSAADA

HAKUNA MICHANGO YA KISIASA AU YA KIDINI

SGS inatekeleza sera kali ya kutoegemea upande wowote katika mchakato wa kisiasa wa nchi yoyote ambako inafanya biashara. SGS haitoi mchango wa fenda au rasilimali kwa chama chochote cha kisiasa, maafisa waliochaguliwa au wagombeaji ofisi za umma katika nchi yoyote, na haiungi mkono kampeni yoyote ya kisiasa. SGS haiungi mkono shirika lolote la kidini.

MICHANGO YA KIMSAADA

Michango ya SGS kwa mashirika ya misaada au uwekezaji wa moja kwa moja wa SGS katika miradi isiyo ya faida katika jamii inakoendeshea biashara (ikiwa ni pamoja na usaidizi katika juhudi za msaada wa dharura baaada ya maafa asilia, mchango wa elimu, huduma za afya, utafiti au uwekezaji kama huo na usio na faida) inahitaji idhini ya awali iliyoandikwa kutoka kwa Afisa Mkuu wa Uendeshaji wa SGS aliye na wajibu wa eneo husika. Michango ya misaada zaidi ya CHF 10,000 inahitaji idhini ya awali ya Kamati ya Maadili ya Kitaaluma ya SGS.

Idhini ya aina yoyote ya michango ya kimsaada haitatolewa kama inakusudiwa au inaonekawa kushawishi maafisa wa serikali au watu wa tatu ili waipatie SGS manufaa yasiofaa.

ZAWADI NA BURUDANI

MAADILI YA MSINGI

Hakuna zawadi, ukarimu au burudani zinafaa kupeanwa au kuchukuliwa kama zinashawishi kwa njia isiyofaa au zinaonyesha kama kuna ushawishi usiofaa katika uamuzi wa biashara.

Zawadi, ukarimu na burudani hazitazidi zile huwa katika uhusiani wa kawaida. Aina yoyote ya burudani inayowezakuwa na uharibifu wa sifa ya SGS lazima iepukwe. Sheria zifuatazo zinabainisha kiwango cha tabia kinachotarajiwa kutoka kwa wafanyikazi wa SGS.

Washirika wanaweza kuongeza sera zenye maelezo na vikwazo zaidi kwa wafanyikazi wao, wakizingatia hali ya mahali.

ZAWADI ZINAZOPEWA WAFANYIKAZI WA SGS

Wafanyikazi wa SGS wasiwahi kukubali:

- Malipo ya pesa taslimu, bahshishi, mikopo, zawadi linganifu na pesa taslimu kutoka kwa wagawaji au wateja.
- Zawadi, mapendeleo, burudani au ukarimu wowote wa kibinafsi zinapopatianwa zikihusiana na huduma iliyofanywa na SGS.
- Wafanyikazi wanaohusika na uamuzi wa ununuzi au uchaguzi wa wagawaji wasikubali zawadi za kibinafsi zinazotolewa na wagawaji au wagawaji wanaotazamiwa. Kwa kawaidia ukarimu na burudani, ikiwani pamoja na kushiriki katika maonyesho ya biashara na matukio kama hayo ya kitaalamu yanayodhaminiwa na wagawaji, kunakubaliwa, mradi kunaambatana na wajibu wa kuripoti na kukubaliwa.

WAJIBU WA KURIPOTI NA IDHINI

Wafanyikazi wanapaswa kuripoti na kutafuta idhini ya awali kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa mshirika wa SGS kabla ya kukubali zawadi yoyote ya thamani zaidi ya CHF 100. Kwa zawadi za thamani zaidi ya CHF 500 lazima wapate idhini ya Afisa Mkuu wa Uzingatiaji wa SGS.

Kama zawadi zilizopokewa haziwezi kukataliwa au kuregeshwa bila ya kuzua chuki, mtu anayepokea zawadi anafaa achague utaratibu mzuri wa kuziondoa mikononi mwake, kwa mfano mchango kwa shirika la msaada lililochaguliwa.

ZAWADI ZINAZOPEANWA NA SGS KWA MAHUSIANO YA KIBIASHARA

Zawadi za kibinafsi zinazopeanwa na SGS kwa wateja au mahusiano ya kibiashara zinahitaji idhini ya awali kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa mshirika wa SGS kwa zawadi yoyote yenye thamani zaidi ya CHF 100, na ikizidi, kwa zawadi za thamani zaidi ya CHF 500 lazima wapate idhini ya Afisa Mkuu wa Uzingatiaji wa SGS.

Kutaka kulipia usafiri na malazi ya maafisa wa serikali au washirika wa biashara katika matukio yaliyodhaminiwa na SGS, au kwa madhumuni ya kuzuru shughuli ya utendaji ya SGS, kunahitaji idhini ya awali ya wajumbe wa Halmashauri ya Uendeshaji (kimsingi COO mmoja na EVP mmoja). Kama gharama ya usafiri na malazi hayo itapita thamani iliyosawa na CHF 10,000, idhini ya Afisa Mkuu wa Uzingatiaji wa SGS itajitajika.

USHINDANI WA HAKI

SGS inafanya biashara yake kwa kutumia njia za ushindani zilizo za haki sokoni. Haijishughulishi na uelewano wowote au makubaliani yoyote na washindani yaliyo na matokeo ya upendeleo au ushawishi usiofaa wa masoko yale inafanyia biashara zake.

Hasa, SGS haijishirikishi katika mijadala kuhusu upangaji bei, makubaliano ya mikataba, ugawaji wa soko, ugawaji wa maeneo au wateja. SGS haijadili michakato ya zabuni ya ushindani na washindani.

SGS haitangazi huduma na uwezo wake kwa njia iliyo ya udanganyifu au kupotosha, na haitoi madai ya umbua au yasio ya kweli kuhusu washindani.

SGS haitafuti habari ya siri kuhusu washindani kwa kutumia njia zisizo halali au zisizo za uadilifu.

Sheria zinazosimamia ushindani ni ngumu na zinabadilika kulingana na maeneo. Ushauri unafaa kutafutwa kutoka kwa rasilimali za kisheria za SGS.

UHUSIANO WA MFANYIKAZI

HAKUNA UBAGUZI

Wafanyikazi wote wa SGS lazima watendewe na watathminiwe kwa ujuzi wao wa kikazi, hitimu, tabia na utendaji wao peke yake. SGS inakadiri vipengele vyote vya uhusiano wa ajira kwa maadili ya fursa sawa kwa wote, bila kuangalia mbari, rangi, dini, mwegemeo wa kisiasa, uanachama wa chama cha umoja wa wafanyikazi, utaifa, ujinsia, asili ya kijamii, umri au ulemavu. Ubaguzi kwa sababu ya vigezo hivi haukubaliwi.

UONEVU NA UNYANYASAJI WA KIJINSIA

Aina yoyote ya dhuluma, unyanyasaji na uonevu hairuhusiwi. Utongozaji wa lazima, kuomba vitendo vya ngono au kugusana kimwili kusikofaa hakuruhusiwi. Wafanyikazi wote wanatarajiwa kuwatendea wafanyikazi wenzao kwa heshima. Wafanyikazi lazima wawe wa kweli na wenye heshima wakati wote katika shughuli zao na wafanyikazi wao, wenzao na usimamizi. Hii pia inawahusu wateja wa SGS, wagawaji, wafanyikazi na usimamizi wao.

MAKATAZO YA AJIRA YA WATOTO AU AJIRA YA KULAZIMISHWA

SGS haiajiri watoto chini ya umri wa kumaliza masomo ya lazima au, kwa hali yoyote ile, chini ya miaka 16. Wakiajiriwa, wafanyikazi wachanga kati ya umri wa miaka 16 mpaka 18 wanalindwa kutokana na aina yoyote ya kazi inayoweza kudhuru afya yao, ustawi, usalama au elimu yao.

SGS haijishirikishi katika aina yoyote ya utumwa, uuzaji au usafirishaji wa watoto, utumwa wa deni au ujakazi, ajira ya kulazimishwa au ya lazima. SGS haitumii kwa hali yoyote ile aina yoyote ya ajira ya kulazimishwa, ya kufungwa au ya gereza.

UHURU WA KUSHIRIKANA

SGS inatambua haki ya wafanyikazi wake ya kuunda nakujiunga na vyama vya wafanyikazi na kuafikiana kwa pamoja. Katika hali ambayo haki ya uhuru wa kushirikiana au kuafikiana kwa pamoja inezuiwa na sheria, SGS inarahisisha njia sawa za uhuru na ushirikiano wa huru na kuafikiana. Wawakilishi wa wafanyikazi wanapata muda na vitu vinavyohitajika kufanya shughuli zao.

UZINGATIAJI WA WAGAWAJI NA MAKANDARASI WASAIDIZI

SGS haitumii wagawaji au makandarasi wasaidizi wanaotumia ajira ya kulazimishwa au ajira ya watoto, na inafanya juhudi na kufuatilia kunakohitajika ili kuhakikisha kwamba wagwaji na makandarasi wasaidizi wanazingatia mahitaji haya.

MAZINGIRA, AFYA NA USALAMA

MAZINGIRA

SGS inajitahidi kupunguza madhara ya shughuli zake katika maringira kwa kuhamasisha matumizi mazuri ya maliasili, upungzaji na uzuiaji wa uchafuzi wa mazingiria na upunguzaji wa utoaji wa vitu hatari na uzalishaji wa gesi za viwandani.

AFYA NA USALAMA

Wafanyikazi lazima wapewe mazingira, hali na vifaa salama vya kufanyia kazi na kuwe na hatua zinazofaa ili kuzuia majeraha na magonjwa yanayohusiana na kazi.

Wafanyikazi wa SGS wanatarajiwa kuripoti na kunakili ajali yoyote inayohusiana na kazi au tukio la uchafuzi wa mazingira kama inavyohitajika na sera za au sheria husika SGS. Hakuna mfanyikazi ataadhibiwa kwa kutoa ripoti kuhusu ajali au tukio la uchafuzi wa mazingira.

USIRI

SGS inaheshimu na kulinda habari za siri walizokabidhiwa na wateja na watu wa tatu katika ile hali ya biashara na inachukua njia zinazofaa kuzuia ufichuzi wa bahati mbaya.

SGS inaheshimu hali ya faragha na ya siri ya habari za kibinafsi za wafanyikazi wake. SGS inachukua na kuiweka data ya kibinafsi ya wafanyikazi, wateja na wambia wa biashara kwa kiwango kinachohitajika katika utendaji bora wa biashara yake au uzingatiaji wa mahitaji ya sheria peke yake. Hakuna mfanyikazi anapaswa kujaribu kufikia data ya kibinafsi au ya siri, ila tu kwa sababu ya madhumuni ya biashara halali.

Wafanyikazi wanafaa wadumishe usiri wa habari ya SGS na data ya kibinafsi ya wafanyikazi wenzao na wasifichue au kujadili habari yoyote nyeti kuhusu utendaji wa kifedha wa SGS, uwekezaji, mikakati, mipango au wateja. Jukumu hili linaendelea hata baada ya mwishowa uhusiano wa ajira.

UVUMBUZI

SGS inaulinda uvumbuzi wake na inaheshimu uvumbuzi wa wengine.

Kupitia kazi na uwezo wa ubunifu wa wafanyikazi wake, SGS inazalisha fikira, huduma, michakato ya biashara na mikakati iliyo na thamani. Uvumbuzi huu unasaidia sana katika uzalishaji wa faida ya ushindani na lazima ulindwe kutokana na usambazaji na utumizi mbaya.

Uvumbuzi wa SGS unaweza kuchukua mitindo mingi, ikiwa ni pamoja na michakato, miundo, mbinu, utaratibu wa uendeshaji, mikakati ya kibiashara na uuzaji, habari za wateja, bei na njia ya kuripoti gharama. Wafanyikazi hawapaswi kufichua, kunakili au kutumia uvumbuzi huu isipokuwa tu kwa madhumuni yake yaliokusudiwa.

Wafanyikazi wanafaa pia kuwa na uangalifu huo wanapofichuliwa uvumbuzi wa wateja.

SGS haiingilii uvumbuzi wa watu wa tatu kimaksudi. Utumizi wa programu isiyokuwa na kibali, utumizi au unakili wa nyenzo zenye hakimiliki bila ya idhini au kuvunja hataza halali kimaksudi kumekatazwa.

MAWASILIANO YA NJE

SGS ni kampuni ya umma na iko chini ya wajibu wa kutangaza kunakokusudiwa kutawaruhusu wawekezaji kufanya maamuzi ya uwekezaji kwa wakati muafaka na wakiwa na habari inayohitajika. SGS inatoa taarifa iliyothabiti, sahihi, ya wazi na dhahiri kwa wenye hisa na wawekezaji wake, kwa soko na kwa jamii yote kwa ujumla kuhusu biashara na shughuli zake. Mawasiliano kwa wenye hisa, wawekezaji, vyombo vya habari na kwa umma kuhusu SGS, biashara yake na utendaji wake wa kifedha, yanafaa kufanywa na watu walioidhinishwa peke yake.

Hakuna mfanyikazi ataongea kwa niaba ya SGS, atajadili au kufichua habari yoyote kuhusu SGS kwa vyombo vya habari, wachambuzi wa kifedha, kwa wawekezaji wa sasa au wawekezaji wanaotazamiwa, au kutoa taarifa ya umma kwa niaba ya SGS ila tu idhini hasa ya kufanya hivyo iwe imetolewa.

Maoni ya kibinafsi, kwa upande wa dini na siasa, au aina yoyote ya maudhui yasiyokubalika hayawezi yakaelezwa katika barua yenye jina na anwani ya SGS, barua pepe ya SGS au kwa hali ingine ile pale maoni kama hayo au nyenzo hizo zinaweza zikaonekana kama zimetolewa na SGS.

Wakati wanashiriki katika majukwaa ya majadiliano ya mtandao na vyombo vya ushirikiano vya mtandao, wafanyikazi wa SGS lazima wazingatie Kanuni za Uadilifu na Sera za SGS za Vyombo vya Ushirikiano.

UUZAJI HISA USIOKUWA HALALI

Wafanyikazi hawapaswi kufukuzia uwekezaji wowote wa kibinafsi au fursa zozote za biashara kwa kutegemea taarifa isiyo ya umma inayohusiana na SGS, wateja wake au wagawaji.

Wafanyikazi wamezuiwa kuuza hisa, chaguo na mafungo mengine yaliyotolewa na SGS wakiwa na taarifa ya ndani isiyo ya umma ambayo, kama itafichuliwa, inaweza kubadilisha bei ya hisa za SGS. Taarifa isio ya umma kama haijatolea rasmi na SGS kulingana na sheria za soko la hisa.

Taarifa ya ndani kwa kawaida ni pamoja na matokeo ya kifedha yasio ya umma, maandiko ya mipango muhimu ya Kundi, mapendekezo ya ununuzi na miungano, mabadiliko yaliopangwa katika usimamizi wa ngazi za juu. Ushauri unafaa kuuliziwa kutoka kwa rasilimali za kisheria za SGS kabla ya biashara ya aina yoyote ambayo inaweza kuwa katika kundi hili.

Katika mfululizo wa baishara yake, wakati mwingine SGS hupata taarifa muhimu isiyo ya umma kuhusu wateja au watu wa tatu. Wafanyikazi wamekatazwa kuuza hisa za wateja au watu hao wa tatu wakiwa na taarifa hiyo ya siri.

Ni halali kupatiana taarifa hiyo, au kupeana vidokezo vya uwekezaji kwa watu wa tatu au jamaa wa karibu kwa msingi wa ujuzi wa ndani uliopatikana wakati wa ajira na SGS.

UZINGATIAJI WA SHERIA

SGS inazingatia sheria zinazohusika katika nchi zile inafanyia biashara. Sheria zilizotungwa zinazohusika na vipengele mbalimbali vya shughuli za SGS zinaweza kuwa ngumu. Wafanyikazi wanahitaji kujua sheria zinazohusika na SGS na kwao kama watu binafsi. Kama kuna tashwishi, ushauri wa kisheria unafaa utafutwe kutoka kwa rasilimali za kisheria za SGS. Kutojua sheria sio kisingizio.

Wakati Kanuni hii au sera za SGS zinaweka vikwazo vikali zaidi kuliko vile vinavyohitajika na sheria husika, wafanyikazi lazima wa zingatie vikwazo hivyo vikali zaidi. Wakati kuna tashwishi ya vipi kutatua ukinzani kati ya Kanuni hii na sheria husika, wafanyikazi wanafaa waombe ushauri.

Katika mfululizo wa biashara ya SGS, mashirika ya udhibitishaji au maafisa wa serikali wanaweza kuwasiliana na wafanyikazi kuhusu uchunguzi unaohusu SGS. Katika tukio la maombi ya taarifa au nyaraka yasiyo ya kawaida, wafanyikazi wanapswa kuuliza ushauri kutoka kwa rasilimali za kisheria za SGS. Hakuna hali yoyote ile inamruhusu mtu yoyote anayetenda kwa niaba ya SGS kujaribu kupotosha, kuficha ushahidi, kuharibu nyaraka au vinginevyo kuzuia uchunguzi wowote wa halali.

UTEKELEZAJI

Kanuni za Uadilifu ilikubaliwa na Halmashauri ya Uendeshaji na Bodi ya Wakurugenzi wa SGS. Kamati ya Maadili ya Kitaaluma ya Bodi ya Wakurugenzi hupokea ripoti za mara kwa mara kuhusu uvunjaji na inasimamia utekelezaji wake.

Kanuni itaanza kutumika kuanzia mwezi wa Februari 2012 na ichukue nafasi ya toleo lililotangulia la 2004.

Washirika wa SGS wamekubaliwa kuchukua sera zenye maelezo zaidi au vikwazo zaidi katika sehemu zilizoelezewa na Kanuni hii, wakiwa na idhini ya awali iliyoandikwa kutoka kwa Afisa Mkuu wa Uzingatiaji wa SGS.

MAELEZO YA MAWASILIANO

MAWASILIANO YA UZINGATIAJI

1 place des Alpes

P.O. Box 2152

CH – 1211 Genève 1

Schweiz

t +41 (0)22 739 91 00

f +41 (0)22 739 98 81

integrityhelpline.sgs.com

www.sgs.com

Shukrani za dhati kwa wafanyikazi na washika dau wote kwa mchago wao uliosaidia kutengeneza Kanuni zetu za Uadilifu.

WWW.SGS.COM

© 2019 SGS SA. HAKI ZOTE ZIMEHIFADHIWA.

WHEN YOU NEED TO BE SURE

SGS